NDUGU ALI Said Salim Mansur Maully wakati wa kukoroga na kupika halua katika sufuria la kitamaduni la karne nyingi kutoka Oman.

# WAISILAMU WAILANI ISRAEL KUHUSU JERUSALEM

BARAZA KUU la Waisilamu Pwani nchini Kenya limepitisha azimio la kuilani Israel kwa upanuzi wake wa mipaka na kufanya Mji wa Jerusalem makao makuu ya Israel.

**na SALEH A. AL-ISMAILLY**

Katika taarifa ya azimio hilo kutokana na kikao cha dharura cha baraza hilo katika Islamic Centre mjini Mombasa azimio hilo vile limetoa mwito kwa Umoja wa mataifa kutwaa hatua zinazofaa kwa haraka ili kuokoa mji wa Jerusalem wenye makao makuu ya kidini katika "Uisilamu (Masjid Al-Aqsa) na katika ukristo makao muhimu matakatifu usikabiliwe na mabambano ya makombora ya kivita.

Katika kikao hicho cha tarehe 7 Septemba, 1980 azimio pia lilipitishwa kwa makao makuu ya Umoja wa Mataifa kujadili swala hilo ambalo litazidi kuhatarisha amani katika mashariki ya kati na kuhatarisha amani ya ulimwengu.

Azimio hilo pia lilitoa mwito kwa serikali ya Kenya na Mkuu wa Mkoa wa Pwani kutwaa hatua kupambana na ongezeko la utumizi wa madawa ya ulevya kama vile Bangi na mira kati ya vijana na wasichana wa Pwani, na ongezeko wa madawa ya aina nyingi yanayoingizwa humu nchini kutoka mataifa ya Ulaya.

Katibu mtendaji wa Supkem Sheikh Mohammed Amana alitangaza orodha ya ziara zake humu nchini.

Mwezi wa tisia atatembelea sehemu za Wilaya ya Kwale kama Kinango, Lungalunga, Kikoneni, Shimoni, Msambweni Tiwi na Mombasa kuanzia tarehe 19 mpaka tarehe 23.

Taita Taveta kuanzia tarehe 24 kupitia sehemu za Taveta, Voi, Kilifi na Malindi mnamo tarehe 27 na 28 saa nne asubuhi.

Hola huko Tana River mnamo tarehe 30 na Mororo tarehe 1/10. Sehemu za North Eastern Garissa mnamo 2/10, Modogashe 3/10, Wajir 5/10 na Mandera 7/10.

Sheikh Mohammed Amana alisema lengo la ziara hizo ni kuona maendeleo, kubadilishana mawazo, na kuuhutubia umma wa Kiisilamu.

# WAOMAN WADUMISHA UPISHI

JEE wajua halua ni kitu gani? Halua ni upishi wa kitamaduni kutoka mataifa mengi ya mashariki ya Kati na hata ghuba ya Arabuni sehemu za Oman, Muscat, ambako Waarabu wa sehemu hizo walifika hapa kwetu miaka na karne kadha zilizopita.

Msimamizi mkuu wa kazi hizo Mombasa ni Sheikh Mansur Seif bin Ali Al-Husni, mzalia wa Mombasa, na ndugu pamoja na watoto akina Ali Said bin Salim Mansur Al-Maully wote maarufu sana mjini Mombasa sehemu za Bondeni.

Marehemu Mzee Seif bin Ali Husni (Simba wa Mombasa) aliwaachia watoto urithi huu wa Halua: Biashara na upishi ambao ni maarufu sana.

Ndugu wengine akina Nassor Salim Mansur Al Maully ambaye ni hivi majuzi tu ambapo alitwaa hatamu za biashara hiyo baada ya kifo cha marehemu baba yake Mzee Salim Mansur Al-Maully.

Halua kwa ufupi inatokana na Unga wa aina ya Uwanga (Wanga), ambao hupigwa na kufurugwa pamoja na lozi, samli safi kabisa, iliki, na vifaa kadha muhimu vya upishi ambavyo ni siri havitajwi hadharani, na kutiwa katika sufuria kubwa la haluwa na kukorogwa mpaka kuiva vile inavyohitajika.

Halua ni chakula cha kutia nguvu, chenye ladha ambayo ni ya pekee, na ni chakula kati ya vyakula vizuri mno vinavyotia tita na nguvu za kiwiliwili chote.

Lakusikia si la kuona na halua ufahamu ni za aina nyingi. Usione kuwa halua ni za aina moja. Kwa hapa Kenya Wa-Oman wenyewe akina Sheikh Mansur Seif bin Ali Husni na Sheikh Nassor Salim Mansur Al-Husni ndio wa pekee wanaotengeneza halua zilizo-halua.

Hebu jaribu kuwaona. Hivi leo Sheikh Mansur Seif al-Husni alisema na *COASTWEEK* "Halua yetu imepata sifa kubwa Afrika na hata Oman, na wageni wengi hufika hapa kuinunua na kuisafirisha nje".

*NDUGU ALI Said Salim Mansur Al-Maully akipima kipande cha halua huku akiangaliwa na jamaa zake, Bondeni, Mombasa . . . . Karibu yake ni Sheikh Mansur Seif al-Husni.*

# MATESO YA UGANDA NA MSIMAMO WA KENYA

UGANDA BILA ya shaka ni taifa huru, na ni taifa la wananchi wa Uganda wote, wa makabila yote. Utawala wa Idi Amin Dada ulilaaniwa sana na Waganda, na walisaidiwa na Tanzania kumuondoa Idi Amin Dada na dhuluma zake zote pamoja na mateso aliyotesa wananchi wa Uganda na mauaji. Hali hiyo pia ililaaniwa na wananchi wote wa Kenya, pamoja na viongozi wetu wapenda amani, umoja na maendeleo, na pia ulimwengu mzima. Visa vya ukatili na hatari ya maisha havikumalizika nchini Uganda baada ya kuondolewa Idi Amin Dada, hayo hayakuwa matumainio ya wananchi wa Uganda na hata ulimwengu mzima pamoja na nchi jirani kama Kenya.

Uganda ilimwaga damu nyingi kutosha wakati wa Amin, wakati wa sababu za mapinduzi za kumuondoa Amin, na baada ya mapinduzi ambayo mpaka sasa hayajaweza kudhibiti taifa la Uganda na kuzuia roho zaidi zisiteketee nchini humo.

Wasio na hatia wanapozidi kupigwa risasi na kuangamia ni lazima ulimwengu upige kelele kuwatetea, wao wakiwa Waganda au si Waganda raia wa nchi nyingine ni lazima ulimwengu uwatetee. Leo itakuwaje Kenya ina makosa wakati ikisema ukweli? Jee si kweli maisha ya watu wa Uganda yanakabiliwa na meteso, mauaji, na ukatili usio kifani? Jee si kweli watu wasio na hatia wanakabiliwa na vifo? Jee si kweli hali mbaya ya chakula na mauti yanatokea nchini Uganda?

Uganda ni sehemu ya ulimwengu, sehemu ya Afrika, na sehemu ya Afrika Mashariki, na sehemu ya nchi jirani yenye uhusiano wa karne nyingi na Kenya na mataifa yote ya Afrika Mashariki. Haitakuwa kiungwana, wala kibinadamu ikiwa Kenya na kiongozi wetu Mtukufu Rais Daniel Arap Moi itanyamaza kimya na kufumba macho na masikio kuhusu mauaji na ukatili unaoendelea nchini Kenya. Mtukufu Rais Moi, kiongozi wetu mwenye imani, na mcha Mungu kila mara yuwatoa mwito kwa Uganda na viongozi wa Uganda kufikiria hatua nzuri za kukomesha mauaji nchini Uganda, kutwaa hatua za kuleta umoja kati yao, mapenzi kati yao na kusimamia Taifa lao bila chuki wala kulipiziana kisasi. Lakini baadhi ya viongozi wa Uganda waliovishwa vilemba vya ukoka wana tafsiri nyingine kabisa kuhusu maoni hayo ya Kenya na viongozi wa taifa hili.

Waganda wote yafaa wafahamu jirani mwema ni yule anayekupa mawaidha mema, jirani asiyekuwa mchochezi au muangamizi. Ni sifa ya Kenya na uwongozi wa Mtukufu Rais wetu mpendwa, muadham Daniel Arap Moi kuzidi kuimarisha na kudumisha ujirani mwema, tunalowatakia Waganda wote ni amani nchini mwao, umoja, furaha na maendeleo. Sisi kwetu Kenya wanaweza kupata faida kubwa wakifuata Maongozi ya Nyayo yaliyobuniwa na Rais Moi. Anayekupendelea amani usimtaje kwa ubaya, kwani yanayotokea Uganda leo hayapo katika siri ulimwengu mzima umekodolea macho Uganda kwa hivyo ni juu ya Waganda wote kudumisha mwenendo wa kuwapatia sifa nzuri.

# Balozi Mgeni wa Heshima

**BALOZI WA Saudi Arabia nchini Kenya Sheikh Jamil Abed Tahir atakuwa mgeni wa heshima katika sherehe za kuadhimisha mwaka wa mia moja wa msikiti wa Nasserpuria Memon Jamat mnamo tarehe 20/9/80.**

**Taarifa rasmi ya mipango ya sherehe yasema kwamba sherehe zitaanza saa kumi na robo jioni. Sherehe hizo pia zitahudhuriwa na wawakilishi kutoka vyuo vya Kiisilamu na wakuu kutoka kote nchini.**

*BALOZI wa Saudi Arabia Kenya Sheikh Jamil Abed Tahir.*

# DINI YA KIISLAMU NA LUGHA

MAONGOZO ya dini ya Kiisilamu yote yamo katika Quran tukufu. Quran yenyewe imeteremka katika lugha ya Kiarabu. Kwa hivyo lugha ya dini yetu ya Kiisilamu ni Kiarabu.

Inavyoelekea, ni kwamba dini ya Kiisilamu ifunzwe kwa lugha ya Kiarabu. Hivi karibuni, alikuja kiongozi wa Mabohora na shekhe wao Seyyidna Burhanudin hapa nchini Kenya.

Katika moja wa hafla za dini alizohudhuria, alitamka kwamba Kiarabu ndiyo lugha ya dini yetu kwa hivyo Waisilamu wote wajitahidi wajifunze lugha hii.

Huu ni mwito w maana sana na unaweza kuitikiwa.

Lakini pamoja na hayo, kuna aibu mkubwa kuona wako Waisilamu wanaojua Kiarabu vyema na Kiswahili vyema lakini hawawezi kuzitumia lugha hizi kwa kumfundishia mtu dini mpaka watumie Kiingereza na ilhali hawa ni wakaazi wa Mwambao wa Pwani.

Ni wataalamu sampuli hii ambao hutayarisha taratibu za kufundishia dini ya Kiisilamu mashuleni kwa Kiingereza. Kwa nini?

Mitihani ya vidato vyote ya dini ya Kiisilamu hutungwa kwa Kiingereza. Na wanaokwenda kuisahihisha mitihani hii, ni wale wale Ali na Omar na Breik kwani wao ndiwo waalimu wa somo hilo. Baba yangu mimi ni mwanazuoni.

Ukimpa maswali ya mitihani itungwayo kwa Kiingereza, hataweza kujibu hata suala moja. Jee babaangu haijui dini yake? Wanafunzi wanaosomeshwa dini katika vyuo vikuu vya Madina na Azhar hutumia lugha gani?

Wanazuoni wetu wote wa sehemu za Magunyani wanajua lugha mbili Kiarabu na Kiswahili, na wanatumia lugha hizo kufundishia katika madrasa zao.

Wala hatumjui shekhe wa Kiisilamu atakae kusomesha tafsiri na Khadithi za Mtume wetu kwa Kiingereza. Sasa Kizungu hichi katika Uislamu kimezuka wapi?

Waliohusika wataka wafanye haraka kuchagua lugha ya dini yetu. Kwani vitabu vya kusomeshea dini ya Kiislamu hupasihwa Al Azhar na Madina wala siyo Oxford na Cambridge.

**Said Burhan,**
**MOMBASA.**

## SAUTI ZA WASOMAJI

**COASTWEEK** Sanduku La Posta 87270 Mombasa KENYA

# SAUTI YA MVITA

TWAOMBA NAFASI ya kutoa malalamiko na kumuunga mkono waziri wa habari na utangazaji Bw. Aringo pamoja na Mhariri wa COASTWEEK kuhusu Sauti ya Mvita. Radio hiyo tokea kuondoshwa Pwani sasa tumekabiliwa sana na porojo chafu kutoka Tanzania na Somalia. Twaomba serikali yetu irudishe Sauti ya Mvita Mombasa ili tuweze kupambana na Radio za Tanzania na Msomali. Radio za Tanzania na Somali hazitafua dafu ikiwa Sauti ya Mvita itapewa uwanja wake kutumikia watu wa Pwani kulingana na Dini yao, Utamuduni wao na hata ufasaha wa lugha ya Kiswahili.

**Ali Kibwana, Faraj Abeid, Abdalla Mwanjaa, Salima Mtawa, MOMBASA.**

**Coastweek** ★★

## SWAHILI CROSSWORD NO. 95



*KWENDA KULIA:*

1. Aina ya gari
5. Haina kasoro
8. Pesa za zamani
9. Mwenda tezi na . . .
10. Iliyonenepa
13. Utandikeni, uchapeni
16. Siyo, hapana
17. Iba
18. Cha kujianglia

*KWENDA CHINI:*

1. Mmea wenye thamani
2. Wilaya moja ya Pwani ya Kenya
3. Maji ya nazi
4. Mimi
5. Namna ya taa
6. Kama kombamwiko
7. Tamka la kushtuka
11. Mchezo wa kitoto
12. Namna ya samaki wa bahari
14. Sehemu, fungu
15. Kiungo cha maneno

JINA

SANDUKU LA POSTA

JEMBE
UNGA SAFI NO. 1
WA MAHINDI

**Washindi wa Fumbo la Kujaza Maneno No. 93:**

[1] Miss Rosemary M. Meshack, Sanduku la Posta 52, Kajiado,

[2] Miss Njeri Kabao, Sanduku la Posta 84126, Mombasa,

[3] Mrs Esha Said, Sanduku la Posta 87010, Mombasa.

Washindi waombwa wafike afisini mwa *COASTWEEK*

**MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO. 93 —**

*KWENDA KULIA:*

1. UNGALIKO, 6. UTO, 7. UNDANI, 8. ZAA, 10. BIRIANI, 13. OA, 14. PA, 16. KWALE, 17. ZEZE, 19. AU, 20. KOMAA.

*KWENDA CHINI:*

1. UTUMBO, 2. GODORO, 3. LINDA, 4. KU, 5. OTEA, 8. ZI, 9. AFA, 11. IAKE, 12. NDARO, 14. PERA, 15. MEA, 18. ZU.

**Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:**

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa.

Washindo watatu wa kwanza kila mmoja atapatiwa 'T'-shirt moja ya Jembe.

Shindano hili limedhaminiwa na *COASTWEEK LTD* pamoja na ATTA LTD, Mombasa.

Jawabu za fumbo hili lipelekwe kwa Muhariri, *COASTWEEK*, Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya. Siku ya Alhamisi tarehe 18.9.80 saa sita mchana shindano hili litakuwa mwisho.